

**MKATABA WA KUPANGISHA GHALA NA YADI YA KUEGESHA MALORI  
YA MIZIGO**


**KATI YA**

**NODO TANZANIA COMPANY LTD  
(MWENYE GHALA NA YADI)**

**NA**

**STALWART ILMA TANZANIA LIMITED – (MPANGAJI)**

**KATIKA NYUMBA ILIYOPO KWENYE KITALU NAMBA 5 & 7, BLOCK EEE,  
HD, IV  
MTAA WA KWA KOMBA – MAJENGO  
KATA YA MJI MPYA  
MANISPAA YA MOSHI  
KILIMANJARO**



**UMEANDALIWA NA:  
WAKILI VICTOR LASWAI  
P.O BOX 1496  
MOSHI - KILIMANJARO**

**MKATABA WA KUPANGISHA GHALA NA YADI YA KUEGESHA MALORI YA  
MIZIGO**

**MKATABA** huu umefanyika leo Tarehe 13 mwezi wa 8 mwaka 2022 kati ya **NODO TANZANIA COMPANY LTD** ya Manispaa ya Moshi, kwa upande mmoja (ambaye katika mkataba huu ataitwa ("**MWENYE GHALA NA YADI**")).

**NA**

**STARLWART ILMA TANZANIA LIMITED** ambaye ni kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sharia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (ambayo katika mkataba huu ataitwa "**MPANGAJI**")

**KWA KUWA** mwenye Ghala na Yadi ni mmiliki wa Ghala na Yadi lililopo katika kitabu namba 5 & 7, **Block EEE**, yenye eneo la **MAJENGO** katika Manispaa ya Moshi na

**KWA KUWA** mwenye Ghala na Yadi ana nia ya kupangisha ghala na Yadi hilo kwa mpangaji huyo; na

**KWA KUWA** mpangaji ana nia ya kupangisha Ghala na Yadi hilo kwa malipo ya kodi na masharti mengineyo yatakayoafikiwa kwenye mkataba huu.

Hivyo basi, mkataba huu unashuhudia na kuthibitisha kama ifuatavyo.

1. **KWAMBA** Mwenye Ghala na Yadi amempangisha Mpangaji Ghala na Yadi hilo lilivyotajwa hapo juu kwa kipindi cha muda wa miaka sita (6) kuanzia tarehe 13 mwezi wa 8 mwaka 2022 hadi tarehe 12 mwezi wa 8 mwaka 2028.
2. **KWAMBA** kiasi cha kodi kitakuwa Tshs. Laki sita (Tshs 600,000/=) tu kwa mwezi na kwamba fedha hizo zitalipwa kwa mwaka Tsh. Milioni saba na laki mbili (7,200,000/=)
3. **KWAMBA** malipo ya fedha za pango yatafanyika kwa njia ya malipo taslimu.
4. **KWAMBA**, ikiwa Mpangaji atatimiza masharti yote ya ulipaji kodi na mengineyo, Mwenye Ghala na Yadi anampgangishia mpangaji ghala na Yadi hilo bila kuwaingilia katika kipindi chote cha upangaji huo.
5. **KWAMBA**, Mpangaji anatakiwa azingatie biashara halali na sio vinginevyo ikiwa ni pamoja na kulipa kodi zinazohitajika na kufanya biashara katika mazingira masafi kama inavyopaswa kisheria.
6. **KWAMBA**, Mwenye nyumba, kwa wakati muafaka anayo haki ya kuingia katika Ghala na Yadi lililopangishwa pale inapobidi ili kukagua au kufanya ukarabati wa Ghala na Yadi hiyo.
7. **KWAMBA**, Mpangaji anatakiwa alipie kwa mwezi, gharama zote za umeme, maji na takataka.
8. **KWAMBA**, Mpangaji haruhusiwi kufanya matengenezo au marekebisho yoyote katika Ghala na Yadi hilo alilopanga bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwenye Ghala na Yadi kwa muda watakaokubaliana wa mkataba huu.

9. **KWAMBA**, Mpangaji haruhusiwi kukodisha ghala hilo alilopanga kwa mtu mwingine yeyote bila ya idhini ya maandishi kutoka kwa Mwenye Ghala na Yadi, na ikiwa Mpangaji atashindwa kuendelea na Mkataba basi mpangaji atamrudishia Ghala na Yadi mwenye ghala.
10. **KWAMBA** Mpangaji amajulishe mwenye Ghala na Yadi kwa maandishi mwanzo wa miezi mitatu ya mwisho ya mkataba huu endapo atapenda kuendelea na mkataba huu mara utakapokwisha.
11. **KWAMBA**, Mpangaji na mwenye Ghala na Yadi wanaweza kusitisha mkataba huu kwa kutoa taarifa kwa maandishi miezi mitatu kabla ya kukatisha mkataba huu.
12. **KWAMBA** Maneno "Mwenye Ghala na Yadi" na "Mpangaji" yatahusu familia, jamii na wategemezi wa kila mmoja wao kwa madhumuni ya mkataba huu.

**KWA USHUHUDA na UTHIBITISHO**, Mkataba huu umewekwa saini na Mwenye Ghala na Yadi na Mpangaji mbele ya Wakili kama inavyoonyeshwa hapa chini:

**IMETIWA SAINI na KUTOLEWA na  
NODO TANZANIA COMPANY LTD** leo hii  
Tarehe 13 mwezi 8 mwaka 2022



Mbele ya:-

**JINA:** VICTOR LASWAI

**Wadhifa:** Wakili

**Saini:**


**Tarehe:** 13-08-2022



**IMETIWA SAINI na KUTOLEWA**

Na **DOUGLAS SAWE MALAMSHA** kwa niaba ya Mpangaji

Leo hii tarehe 13 mwezi 8 mwaka  
2022



**MPANGAJI**

Mbele ya:

**Jina:** VICTOR LASWAI

**Wadhifa:** Wakili

**Saini:**

**Tarehe:** 13-08-2022

